**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO**
**SHULE YA SEKONDARI MATIMBWA**
***"Barua zote zielekezwe kwa Mkuu Wa Shule"***

Simu: +255753012797 AU +255758738225
**Baruapepe** matimbwasecondaryschool@gmail.com

Shule ya sekondari Matimbwa,
S.L.P 130,
Bagamoyo.
Tarehe ……...

---

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATIMBWA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO MKOA WA PWANI MWAKA .......**

## 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ....... na atasoma tahasusi ya ………….

## 2.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Matimbwa ipo katika kijiji cha Matimbwa, kata ya Yombo, tarafa ya Yombo, Wilaya ya BAGAMOYO Mkoa wa Pwani. Umbali wake ni kilometa 15 kutoka makao makuu ya Wilaya ya BAGAMOYO upande wa Kusini Magharibi kandokando mwa njia inayoelekea mji mdogo wa Mlandizi.
Usafiri wa kufika Bagamoyo unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mbezi mwisho au Bunju B jijini Dar es salaam, ambapo basi hilo litakufikisha Bagamoyo mjini. Kutoka Bagamoyo mjini hadi shule ya sekondari Matimbwa unaweza kufika kwa basi dogo (daladala) zinazo toka Bagamoyo mjini kwenda Mlandizi/Mzenga kwa bei ya Tshs 2,000/= au kwakukodi pikipiki kwa Tshs 5,000/= na kushuka kituo cha Miembe saba mahali shule ilipo. Kwa wanao tokea mji mdogo wa Mlandizi, watapanda mabasi madogo (daladala) zinazo tokea Mlandizi kuelekea Bagamoyo na kushuka kituo cha Miembe saba mahali shule ilipo. Wanao toka Kilimanjaro, Tanga na Arusha, watashuka kituo kidogo cha mabasi kichemchem na kuchukua usafiri wa daladala au pikipiki.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe ............., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………... kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:30 jioni.

## 2.1. SARE ZA SHULE:-

**A: KWA WAVULANA:**

- Mashati mawili meupe mapya ya mikono mifupi aina ya tomato.
- T-shirt nyeusi (form six) itapatikana shuleni kwa sh.15,000/= kila moja kwa anayehitaji
- Viatu vyeusi vya ngozi soli fupi vya kupiga rangi na vya kufunga kwa kamba

- Soksi nyeusi jozi tano.
- Suruali pana (siyo bwanga) za 'kijivu' mbili (2) zenye marinda mawili kulia na mawili kushoto mbele.
- Suruali pana (siyo bwanga) za rangi ya maroon mbili (2) marinda mawili kulia na mawili kushoto mbele, kipimo cha chini kisipungue 17 sm.
- Mkanda mweusi wa ngozi usio na nembo ya kihuni wala bakoli nene.
- Aje na T-shirt ya rangi ya dark blue yenye kola (Form six) kwa ajili ya kushindia
- Tai mbili ndefu za rangi ya kijivu.
- Sweta la rangi ya kijivu lenye shingo alama ya V na si vinginevyo.

NB: Ataripoti shuleni akiwa amevaa suruali ya 'maroon' na T-shirt ya rangi ya dark blue yenye kola.

Hairuhusiwi kushona suruali ya kubana na isiyo na marinda (model). Suruali za namna hiyo hazitakiwi kabisa shuleni.

**B: KWA WASICHANA:**

- Sketi mbili rangi ya kijivu mshono wa rinda "box" kubwa moja mbele na moja nyuma na marinda madogo mawili mbele na nyuma kulia na kushoto, urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu kwa ajili ya sare ya shule.
- Mashati mawili meupe mapya ya mikono mifupi aina ya tomato au nusu kanzu inayofika magotini na hijabu nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama, kwa waislamu.
- T-shirt nyeusi (form six) itapatikana shuleni kwa sh.15,000/= kila moja kwa anayehitaji.
- Viatu vyeusi vya ngozi soli fupi vya kupiga rangi, aina ya Juma na Rosa.
- Soksi nyeupe jozi tano.
- Sketi mbili rangi ya 'Maroon' iliyokolea mshono wa rinda box urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu kwa ajili ya kushindia.
- Suruali mbili rangi ya "maroon" zisizobana kwa ajili ya kuvaa usiku kujikinga na mbu wakati wa kujisomea.
- Tai mbili ndefu za rangi ya kijivu
- Sweta la rangi ya kijivu lenye shingo alama ya V na si vinginevyo
- Aje na T-shirt ya bluu iliyo kolea (dark blue) yenye kola (form six) isiyo na maandishi kwa ajili ya kushindia au nusu kanzu ya "dark blue" inayofika magotini na hijabu ya "dark blue" kwa waislamu.

NB:

- Sketi zote ziwe ndefu. Ataripoti shuleni akiwa amevaa sketi ya rangi ya "maroon" na T- shirt ya rangi ya dark blue yenye kola. Kwa waislam wavae sketi ya rangi ya "maroon"na nusu kanzu ya rangi ya "dark blue" na Hijabu ya "dark blue".
- Wanafunzi wote hawaruhusiwi kusuka nywele.

**C. SARE ZA MICHEZO KWA WOTE:**

- Jezi za rangi ya light blue (t-shirt na bukta).
- Tracksuit za rangi ya light blue.
- Wanafunzi wote waje na viatu vya michezo au raba za michezo.

## 2.2 MAAGIZO MENGINE YA SHULE

i. Cheti cha daktari (medical certificate) cha kuthibitisha afya ya mwanafunzi ambayo itajazwa na Hospitali ya Serikali na cheti cha tofauti cha majibu ya vipimo vya TB

ii. Picha sita (6) za'passport size ziwe na 'background ya blue' na vipimo vya sm.4 kwa 4 na awe amevaa sare ya shule wakati wa kupiga picha hizo

iii. Alete picha moja moja ya passport size za wazazi/walezi wake wawili wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu

iv. Madaftari 15 aina ya Counter Book Quire 03 na vifaa vingine vya darasani vya kutosha.

v. Bunda mbili za karatasi nyeupe **(Ream A4 size – aina ya NO.1)** kwa mwaka;

vi. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);

vii. Dissecting tray, nta kilo moja na dissecting kit kwa wanafunzi watakaosoma PCB.

viii. Scientific Calculator (fx-991-ES PLUS) kwa wanafunzi wote isipokuwa HKL zinapatikana shuleni kwa sh. 40,000/= kwa kila moja.

ix. Stopwatch kwa wanafunzi wanaosoma PCM na PCB.

x. Graph pads mbili kwa wanafunzi wote isipokuwa HKL.

xi. Sanduku imara la kuhifadhi mali zake binafsi (tranka).

xii. Godoro la sponji la futi mbili na nusu linapatikana shuleni kwa **52,000/=** kila moja kwa anayehitaji.

xiii. Foronya ya godoro ya ngozi (mackintosh) inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh **35,000/=** kila moja kwa nayehitaji.

xiv. Aje na chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu cha rangi nyeupe.

xv. Shuka jozi mbili za rangi light blue kwa wavulana, na rangi ya pinki kwa wasichana

xvi. Nguo za ndani za kutosha na za kulalia.

xvii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) visiwe vya plastiki.

xviii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.

xix. Aje na tochi kwa ajili ya tahadhari kwa wakati wa usiku (Isiwe ya kuchaji kwa umeme)

xx. Aje na ndala za kuogea na Sandals za kushindia (Zisiwe Crooks).

xxi. Aje na chupa safi kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.

xxii. Aje na Box file kwa ajili ya Portfolio.

xxiii. Sabuni/dawa ya chooni ya maji kwaajili ya usafi wa vyooni lita 05 (aina ya Tarmol).

xxiv. Mwanafunzi aje na kadi ya Bima ya afya kama anayo au aje na Tsh. 50,400 kwa ajili ya kukatia Bima ya Afya shuleni ambayo atatakiwa kuchangia kwa kila mwaka. Hii ni lazima kwa wanafunzi wote.

**2.3 MAHITAJI KWA MAKUNDI**: Mwanafunzi pia atapaswa kuja na vifaa vifuatavyo kulingana na mchepuo wake.

| PCB | PCM | HKL |
|---|---|---|
| Jembe na mpini wake | Reki, squeezer | Panga, Fagio laini |
| Squeezer | Fagio laini | Slesha/Kwanja |

| | | |
|---|---|---|
| fagio la wima wa chelewa | fagio wa wima wa chelewa | fagio wa wima wa chelewa |

### 2.4. MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

### 3.3 .Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi

iii. Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iv. Fomu ya mwanafunzi na mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

v. Picha mbili (02) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

NB:Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MATIMBWA**

**………………………………..**
**ADEOATHA HILARY NKWERA**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule :0753012797**
- **Makamu Mkuu wa Shule -Utawala:0758738225**
- **Makamu Mkuu wa Shule - Taaluma :0715006056**
- **Mwandamizi Malezi :0754927403**

…..…………………………

…..…..……………………….

…..…….…………….…….

Tarehe ……………..

Mkuu wa Shule,

Shule ya sekondari Matimbwa,

S.L.P.  130,

Bagamoyo- Pwani.

**YAH:  KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MATIMBWA**

Nachukua nafasi hii kulishukuru Taifa letu kwa kunichagua na kunipa nafasi ya kupata Elimu ya Sekonari.  Hii ni bahati kubwa na ninaahidi kujifunza kadiri ya uwezo wangu na sitapoteza muda wa masomo darasani au muda wa kazi za mikono kwa kuwa mvivu, au kupuuza shughuli hizo.

Nimesoma sheria za shule na masharti ya kujiunga na shule ya Sekondari Matimbwa na ninakuthibitishia kuwa nimeafiki sheria na masharti hayo na kwamba nitaziheshimu kwa kutokuzivunja kwa makusudi.  Na ikiwa nimezivunja ninastahili kuadhibiwa vikali.

Wako mwanafunzi mtiifu,

…………………………………..

Jina na  Sahihi ya Mwanafunzi

…………………………………..

Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi

NB: Wasilisha fomu hii kwa Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako.

PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTARTION AND LOCAL GOVERNMENT

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

(To be completed by a medical Officer in respect of all form I and 5 entrants)

Student's full name: ........................................................................................

Student's age: ............. Form................

**(To be completed by a government medical officer):**

I have examined the above named student and consider that he/she is fit/unfit for full time studies.

1) Eyesight..............................................................................................................
2) Hearing...............................................................................................................
3) Speech................................................................................................................
4) Limbs..................................................................................................................
5) Venerealdisease.................................................................................................
6) Leprosy...............................................................................................................
7) Epilepsy..............................................................................................................
8) Neurosis..............................................................................................................
9) Asthma................................................................................................................
10) T.B......................................................................................................................
11) Pregnancy...........................................................................................................
12) Diabetes..............................................................................................................
13) Ulcers.................................................................................................................
14) Other..................................................................................................................

**MEDICAL OFFICER'S COMMENTS:**

**.......................................................................................................................................**
**.......................................................................................................................................**
**.......................................................................................................................................**

**Name................................................Signature........................Date..........................Stamp:**

**Station.................................Designation....................................**

**NB:** I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.

**SHULE YA SEKONDARI MATIMBWA**
**FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. JINA ………………………………………………………………………………. DINI ………………………..
2. TAREHE YA KUZALIWA……………………..........3. KIJIJI ULIYOZALIWA……………….......
4. TARAFA ULIYOZALIWA ………………… .......5. WILAYA ULIYOZALIWA ………………....
6. MKOA ULIYOZALIWA …………………………... KAMA UNAKAA MJINI……………........
7. TAJA MJI:………………………….. MTAA………………...BARABARA………………………..
8. JINA LA BABA……………………………...9. KAZI YA BABA…………………………………....
10. ANWANI YA BABA………………………………………………………………………………....
11. JINA LA MAMA …………………………….. 12. KAZI YA MAMA……………………………….
13. ANWANI YA MAMA…………………………………………………………………………..
14. a) JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:
JINA:........................................................... ANWANI:.............................................................
SIMU:.........................................................  EMAIL:............................................................
b) JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:
JINA:........................................................... ANWANI:.............................................................
SIMU:.........................................................  EMAIL:..............................................................

15. SHULE ULIZOSOMA MADARASA MADARAKA ULIYOSHIKA

| | | |
|---|---|---|
| SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA |
| ……………………………. | ………………… | ………………………………… |
| ……………………………. | ………………… | ………………………………. |

16. JE, BABA YU HAI? ……………………………........ (NDIYO/HAPANA)
17. JE, MAMA YU HAI? ……………………………........ (NDIYO/HAPANA)

18. JE, UNAKAA NA MLEZI ……………………………... (NDIYO/HAPANA)

19. ANWANI YA MLEZI …………………………………………………………………
20. KAZI YA MLEZI …………………………………………………………………………
21. ELEZA MATATIZO YA NYUMBANI, YA MAGONJWA, N.K. YANAYOKUKABILI
……………………………………………………………………………………………………

22. UNAFIKIRI MATATIZO HAYO YATATATULIWA VIPI?
………………………………………………………………………………………

23. ELEZA MIPANGO YAKO YA MAISHA YA BAADAYE
…………………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………………………

24. MKO WANGAPI KATIKA FAMILIA? (A) WA KIUME ………………………………………....
(B) WA KIKE ………………………. (C) WEWE NI WA NGAPI ……………………………...
(D) NDUGU WANGAPI WAMEAJIRIWA? ……………………………………………………
25. KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

……………………………………………………………………………………………………….

26. KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

……………………………………………………………………………………………………….

27. JINA ………………………………….. SAHIHI……………………….. TAREHE………………………….

## SHULE YA SEKONDARI MATIMBWA

## MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Ukiwa mwanafunzi na mzazi/mlezi wamekubaliana na masharti yote ya shule, sharti fomu hii isainiwe na watu wanne, ambao ni:

(i) Mwanafunzi mwenyewe:

Jina kamili :.............................................................................................. Kidato:.................

Saini..................................... Tarehe .......................

(ii) Mzazi/Mlezi:
Jina kamili:................................................................... Saini:..............................

Tarehe:.....................................

**VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI**

Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu kulingana na masomo yake kwa kufuata mchanganuo ufuatao.

**A: VITABU:**

| MASOMO | TAHASUSI |
|---|---|
| • PHYSICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL (TIE) STUDENTS' BOOK FORM FIVE.<br>• PRINCIPLE OF PHYSICS (S. CHAND'S) -CLASS XI.<br>• MODERN ABC PHYSICS CLASS XII -PART I<br>• GENERAL AND INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL(TIE)<br>• ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL(TIE)<br>• PHYSICALCHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL (TIE)<br>• MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL (TIE)<br>• HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI SHULE ZA SEKONDARI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO (TIE)<br>• ACADEMIC COMMUNICATION FOR SECONDARY STUDENTS' BOOK FORM FIVE | PCM |
| • PHYSICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL (TIE) STUDENTS' BOOK FORM FIVE.<br>• PRINCIPLE OF PHYSICS (S. CHAND'S) -CLASS XI.<br>• MODERN ABC PHYSICS CLASS XII -PART I<br>• GENERAL AND INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL(TIE)<br>• ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL(TIE)<br>• PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL (TIE)<br>• BIOLOGY FOR AADVANCED SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK FORM FIVE.<br>• BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL (TIE). STUDENTS' BOOK FORM FIVE AND SIX<br>• HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI SHULE ZA SEKONDARI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO (TIE)<br>• ACADEMIC COMMUNICATION FOR SECONDARY STUDENTS' BOOK FORM FIVE | PCB |
| • HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS STUDENTS' BOOK FORM FIVE.<br>• KISWAHILI SHULE ZA SEKONDARI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO.<br>• ENGLISH FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS STUDENTS' BOOK FORM FIVE. | HKL |

| | |
|---|---|
| - **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**<br>**SHULE ZA SEKONDARI**<br>**KITABU CHA MWANAFUNZI**<br>**KIDATO CHA TANO (TIE)**<br>- **ACADEMIC COMMUNICATION FOR SECONDARY**<br>**STUDENTS' BOOK FORM FIVE** | |

**NB: ZIFUATAZO NI BEI ZA VIFAA AMBAVYO VINAWEZA KUPATIKANA MAENEO YA HAPA SHULENI**

| KIFAA | BEI |
|---|---|
| **Godoro** | **52,000/=** |
| **Foronya/ kava ya godoro (ya Ngozi)** | **35,000/=** |
| **T-shirt yenye nembo ya shule** | **15,000/=** |
| **Soft broom, hard broom, squizzer, chelewa, hand broom** | **@3500/=** |
| **Scientific Calculator** (fx-991-ES PLUS) | **40,000/=** |
| **Ndoo ya lita 10** | **5,000/=** |

KIAMBATA CHA RANGI ZA SARE NA SHAMBA DRESS



SHAMBA DRESS (SURUALI AU SKETI)



SARE YA SHULE (SKETI AU SURUALI)